**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.231


# Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati katika Lahaja za Lugha ya Kihaya: Mifano kutoka Kihamba na Kiziba

**Editha Adolph**
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania

**Ikisiri**
Makala hii inafafanua dhana za kufanana na kutofautiana kwa msamiati wa lahaja ya Kihamba na Kiziba katika lugha ya Kihaya. Vipengele vinavyohusika katika kuchunguza kufanana na kutofautiana huko ni vipengele vya tahajia na matamshi. Lengo la ulinganishi na ulinganuzi huo ni kubainisha ikiwa kuna ufanano na utofauti wa kimsamiati unaojitokeza katika lahaja hizi mbili za lugha ya Kihaya yaani Kihamba na Kiziba. Kwa mujibu wa makala hii, eneo hili halijapewa aula na hivyo kumpa mtafiti laghba ya kulishughulikia. Data ya makala hii imekusanywa uwandani katika eneo la Kyamutwala inakozungumzwa lahaja ya Kihamba. Kwa upande wa Kyamutwala, mtafiti amekusanya data katika kata za Kamachumu, Ibuga, Muhutwe na Izigo. Katika eneo la Kiziba data imekusanywa kutoka kata za Buyango, Bugandika, Ruzinga na Bwanjai inakozungumzwa lahaja ya Kiziba. Data hii ya uwandani imepatikana kwa mbinu ya ushuhudiaji, hojaji, usaili na uchanganuzi wa matini za maktabani. Mtafiti alishuhudia namna mbalimbali za kitahajia/hijai na kimatamshi kuhusiana na msamiati wa Kihaya katika lahaja ya Kihamba na Kiziba. Aidha, data ilikusanywa kupitia hojaji ambapo watafitiwa 80 waligawiwa dodoso na kuzijaza kikamilifu. Kupitia mbinu ya usaili, mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na watafitiwa wa makala hii na kuweza kubaini ulinganifu na usiganifu uliopo baina ya msamiati wa lahaja zinazoshughulikiwa katika makala hii. Data ya maktabani ilipatikana kwa mapitio ya matini mbalimbali zinazohusiana na mada inayoshughulikiwa katika makala hii. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba baadhi ya msamiati wa Kihamba na Kiziba hurandana na baadhi husigana. Pia zimetolewa sababau za kufanana na kutofautiana kwa msamiati wa lahaja hizo. Mtafiti wa makala

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-05-09*
*Rekebishwa: 2023-05-30*
*Kubalika: 2023-06-02*
*Chapishwa: 2023-06-07*

***Maneno Muhimu***
Kihaya
Kufanana
Kutofautiana
Lahaja
Msamiati

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Adolph, E., (2023). Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati katika Lahaja za Lugha ya Kihaya: mifano kutoka Kihamba na Kiziba. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(2), 1-16.

*Copyright © 2023*
CC BY NC SA

hii anapendekeza tafiti fuatizi zifafanue kwa kina sababu za kutofautiana na kufanana kwa msamiati wa lahaja hizi tofauti na ilivyoelezewa katika makala hii kwani sababu ni nyingi. Aidha, makala hii itatoa hamasa kwa watafiti kufanya tafiti juu ya lahaja za lugha mbalimbali. Vilevile, makala hii inatoa mchango katika kukuza na kuendeleza lugha za Kibantu na taaluma ya isimu kwa ujumla. Pia itaongeza marejeleo faafu kwa watafiti wa isimu.

## Utangulizi

Lahaja ni tofauti ndogo ndogo zinazojitokeza katika maumbo, matamshi na matumizi ya maneno katika lugha yenye asili moja. (Stigand, 1915; Ingrams, 1924; Trudgill, 1986; Francis, 1992; Romaine, 1994; Mgullu, 1999; Oxford Advanced Learners Dictionary, 2000; Abdalla, 2018). Ikumbukwe kuwa endapo makundi mawili ya watu au zaidi yataelewana bila shida kubwa katika uongeaji wao japokuwa makundi hayo yatakuwa yanatambua upekee wa uongeaji wao, ni dhahiri kuwa makundi hayo ni ya lahaja za lugha moja. Hata hivyo, iwapo makundi hayo hayaelewani kabisa au yanaelewana kwa shida sana, ni dhahiri kuwa makundi hayo ni ya lugha mbili tofauti. Aghalabu, waungumzaji wa lahaja huweza kutofautiana kimatamshi, katika baadhi ya msamiati pia kimuundo na maana (Akmajian, Demers, Farmer na Harnish 2001; O'Grady na Katamba, 2001; Massamba, 2004). Hali hii inadhihirika kwa mfano katika Kiswahili ambacho kina lahaja mbalimbali zenye msingi mmoja wa lugha mama ambayo ni Kiswahili. Lahaja hizo zimeainishwa na wataalamu mbalimbali kama inavyooneshwa hapa chini: Kingare, Kisiu, Kiamu, Kingozi, Chichifundi, Kimtang'ata, Kiunguja, Kimvita, Kingazija, Kimrima, Kihadimu, Kipemba, Kitikuu, Kingwana, Chimbalazi (chimiini), Kivumba, Kimgao na Kitumbatu (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Kundi la lahaja za Kaskazini: Kilindi, Kimvita, Kisiu, Chimiini, Kijomvu, Chifunzi, Kipate, Kibajuni na Kiamu. Kusini: Kimafia, Kihadimu, Kivumba, Kimakunduchi, Kimgao, Kitumbatu, Kimwani, Kipemba na Kimtang'ata Kiunguja na Kimwani (Nurse na Spear, 1985). Kiunguja, Kihadimu, Kitumbatu, Kingozi, Chichifundi, Kingare, Kijomvu, Kiamu, Kimafia, Kisiu, Chimbalazi au Chimiini, Chikomor, Kibajuni, Kimrima, Shindzuani, Kivumba, Kimvita, Shingadzija, Kimwani, Kingazija, Kipate, Kitikuu, Kingao, Kingwana, Kipemba na Kimtang'ata.

Whiteley (1956) amechunguza lahaja ya Ki-mtang'ata. Mtaalamu huyu ameshughulikia masuala mahususi katika kila lahaja kama vile mashina ya maneno pamoja na sifa zinazotofautisha lahaja moja na nyingine. Kupitia utafiti huu, mtafiti amepata mwelekeo wa kuelewa tofauti za kimsamiati za lahaja anazozishughulikia. Tofauti na utafiti wa Whiteley unaochunguza lahaja ya Ki-mtang'ata, mashina ya maneno pamoja na sifa zinazotofautisha lahaja moja na nyingine, utafiti huu unachunguza kufanana na kutofautiana kwa msamiati katika lahaja za lugha ya Kihaya; Kihamba na Kiziba. Kipacha (2003) ameshughulikia tofauti za kimsamiati katika lugha mbalimbali. Mtaalamu huyu anasema kuwa huko Uingereza, suala la tofauti za lahaja kutokana na matabaka linajitokeza sana kutokana na kuwepo kwa tofauti zinazojitokeza kati ya matumizi ya maneno ya tabaka la juu na lile la chini. Tabaka la juu (mamwinyi) linazungumza zaidi lahaja rasmi na lafudhi rasmi wakati lile la chini (wafanyakazi) linatumia zaidi lahaja na lafudhi zenye taathira za vitarafa. Kutokana na maelezo haya anatoa mifano kama vile *headache*, *skill-ache* na *head-work*. Kipacha (ktj) anasema kuwa wazungumzaji wa Kiingereza wa tabaka la juu hutumia zaidi neno *headache* wakati wale wa tabaka la chini hutumia maneno kama *skill-ache* na *head-work*. Anaendelea kufafanua kuwa katika maeneo ya kati ya Uingereza yaani *Midland* si ajabu kusikia neno *dinner* kutumika kwa chakula cha mchana hadi

usiku na hakuna matumizi ya maneno kama *lunch* au *supper*. Hii ni kwa matumizi ya watu wa kawaida. Kipacha anaona kuwa vyombo vya habari kama vile magazeti, televisheni na redio vinajitahidi kusawazisha au kusambaza tofauti za lahaja mbalimbali katika matumizi ya maneno fulani fulani au namna ya utamkaji. Kidogo kidogo yanakuwa yanatumika mara kwa mara katika mazingira rasmi na hivyo kuchukuliwa na wasikilizaji kama ni namna ya utamkaji au ni maneno ya kawaida mfano, *cheers* badala ya *thank you*. Kwa ujumla, tafiti hizi ni muhimu katika makala yetu kwani zimetupa mwanga juu ya kufanana na kutofautiana kwa hali, njeo na msamiati katika lahaja za lugha mbalimbali. Kipacha (2003) alishughulikia tofauti za kimsamiati katika Kingereza. Alijikita katika suala la tofauti za lahaja kutokana na matabaka hususani tabaka la juu na lile la chini. Lakini utafiti wetu unachunguza kufanana na kutofautiana kwa msamiati katika lahaja za lugha ya Kihaya; Kihamba na Kiziba.

Kama alivyomrejelea Stigand (1915), Kipacha (2003) anaeleza kuwa zipo hoja kuwa Kimrima ni lahaja iliyokuwa ikizungumzwa kusini mwa mto Pangani hadi sehemu za Kunduchi karibu na Dar es Salaam. Anaendelea kufafanua kuwa Kimrima kinazungumzwa baina ya Vanga hadi karibu na Kilwa. Anaonesha ushahidi kuwa Kiswahili kilichokuwa kinatumika katika maandishi wakati wa utawala wa Kijerumani kilikuwa katika lahaja ya Kimrima. Kipacha anaonesha tofauti za msamiati wa Kimrima na Kiswahili sanifu kwa kutoa mifano ifuatayo:

| **Kimrima** | **Kiswahili Sanifu** | **Tofauti** |
|---|---|---|
| koka | koga | k:g |
| kalusi | harusi | ka:ha |
| kalama | karama | l:r |
| kwisa | kwisha | s:š |
| singo | shingo | s:š soka shoka s:š |
| kitowero | kitoweo | r:ø |

***Chanzo**: Kipacha (2003)*

Mtafiti huyu amelinganisha pia sifa bainifu za fonimu za Kimrima na Kiswahili sanifu kama ifuatavyo:
(a) /k/ badala ya /g/ mfano: kusokea (kusogea)
(b) /z/ badala ~~ya~~ /š/ mfano: angu-z-a (angu-sh-a)
(c) Urudufishaji ~~wa~~ irabu ndefu mfano: tabu (taabu)
(d) Kutokudondosha konsonanti kati-irabu /r/ ama /l/: mfano: mguru (mguu)
(e) Kutokudondosha irabu ya nyuma juu /u/ baada ya nazali mfano: amuri (amri)
**Chanzo**: Kipacha (2003)

Tofauti na Kipacha anayechunguza tofauti za kileskika kati ya Kimrima na Kiswahili sanifu, utafiti huu unaangalia ni kwa namna gani msamiati wa lahaja za Kihamba na Kiziba zinarandana na kutofautiana. Aidha, utafiti huu umempa mtafiti wa sasa mwanga uliomwongoza katika kuziangazia tofauti za msamiati wa lahaja anazozishughulikia. Kwa mujibu wa Muhura (2009), kuna mambo ya msingi yanayotofautisha lahaja moja na nyingine. Mathalani, msamiati, matamshi, maana ya maneno na hata muundo wake. Aidha, Muhura ameorodhesha lahaja 18 za Kiswahili na kusema kuwa kati ya mambo yanayosababisha lugha moja kuwa na lahaja tofauti ni pamoja na watu kuhamahama, uhaba wa mawasiliano kati ya jamii moja na nyingine pamoja na umbali wa kijiografia. Halikadhalika, Hamad (2018) aliyejikita katika eneo la kulinganisha uwakilishaji wa njeo na hali katika lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi kwa kuzingatia maumbo ya vitenzi vya lahaja hizo. Ili kufikia

malengo yake alilenga kubainisha mofimu za njeo na hali katika Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi na kufafanua kufanana na kutafautiana kwa lahaja hizo katika uwakilishaji wa njeo na hali. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa lahaja zote tatu alizoshughulikia zina idadi sawa ya aina za njeo pamoja na hali. Hamad (2018) anasema kuwa katika uwasilishaji wa njeo na hali, kuna baadhi ya maumbo ya mofimu yamefanana kwa lahaja zote tatu, baadhi yamefanana kati ya Kimakunduchi na Kitumbatu na baadhi yamefanana kati ya Kitumbatu na Kipemba. Mtafiti anaendelea kufafanua kuwa hali hii inasababisha mfanano kuwa mkubwa kati ya Kimakunduchi na Kitumbatu na pia kati ya Kitumbatu na Kipemba huku kukiwa na tofauti kubwa kati ya Kimakunduchi na Kipemba katika vipengele hivyo vya kimofosintaksia vya uwakilishaji wa njeo na hali. Tafiti tangulizi hizi zimeshughulikia lahaja za lugha ya Kiswahili pamoja na lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi tofauti na utafiti huu unaochunguza lahaja za lugha ya Kihaya yaani Khamba na Kiziba. Aidha, vipengele vinavyoshughulikiwa na wataalamu hawa ni mambo yanayosababisha lugha moja kuwa na lahaja tofauti pamoja na vipengele vya kimofosintaksia vya uwakilishaji wa njeo na hali.  Utafiti wa sasa unashughulikia kufanana na kutofautiana kwa msamiati katika lahaja za Kihamba na Kiziba. Tafiti tangulizi zimempa mtafiti wa sasa mwongozo kuwa lugha inaweza kuwa na lahaja tofautitofauti.

**Lugha ya Kihaya na Mahali Inakopatikana**

Data ya makala hii imekusanywa kutoka mkoani Kagera. Kwa mujibu wa Buberwa (2015) mkoa wa Kagera uko Kaskazini Magharibi mwa nchi ya Tanzania, kati ya latitude 1 “00” na 2 “45” Kusini mwa Ikweta na kati ya longitude 30 “25” na 32 “40” Mashariki mwa ‘Greenwich’. Makao makuu ya Mkoa huu yako Manispaa ya Bukoba iliyo umbali wa kilometa 1500 kutoka Dar es Salaam. Aidha, mkoa wa Kagera kwa upande wa Kaskazini unapakana na Uganda, upande wa Magharibi unapakana na Rwanda na Burundi, upande wa Kusini unapakana na Kigoma, Mwanza na Geita, kwa upande wa Mashariki mkoa huu unapakana na Ziwa Victoria. Mutembei (2001) anaeleza kuwa kabla na baada ya kuja kwa wakoloni mkoa huu ulikuwa na utawala wa kichifu uliokuwa na himaya nane; Kihanja (Kanazi), Kiziba, Bugabo, Bushubi, Kyamutwala, Ihangiro, Bukara na Karagwe. Kama tulivyoelezea hapo juu kuwa mkoa huu ulitawaliwa na machifu, wafuatao ni machifu waliotawala maeneo mbalimbali ya mkoa huu: Rukamba → Kyamutwala, Rutinwa → Kiziba, Kayoza → Bugabo, Kasusura → Bushubi, Nyarubamba → Ihangiro, Lugomola → Bukara na Rumanyika → Karagwe. Hivi sasa mkoa huu una wilaya saba; Bukoba Manispaa, Muleba, Bukoba Vijijini, Kyerwa, Misenyi, Ngara, na Karagwe. Lugha ya Kihaya inayoshughulikiwa katika makala hii, inazungumzwa katika Mkoa huu wa Kagera. Lugha hii ina lahaja mbalimbali kama ilivyo katika lugha lugha nyinginezo. Lahaja hizo ni kama vile: Kihamba kinachozungumzwa katika Wilaya ya Muleba maeneo ya Kyamutwala, Kiziba kinachozungumzwa katika Wilaya ya Bukoba Vijijini maeneo ya Kiziba, Kiyoza kinachozungumzwa katika Wilaya ya Bukoba Mjini na baadhi ya maeneo ya Bukoba Vijijini na kadhalika. Kinyaihangiro kinachozungumzwa katika Wilaya ya Muleba maeneo ya Ihangiro pamoja na Kinyambo kinachozungumzwa katika Wilaya ya Karagwe maeneo ya Karagwe.

**Kazi Tangulizi Kuhusu Lugha ya Kihaya**

Tafiti mbalimbali kuhusiana na lugha ya Kihaya zimefanyika, mathalani, (Byarushengo, 1997; Buberwa, 2011; Adolph, 2014; Adolph, 2022; France na Kahigi, 2021;) wamechunguza masuala kadhaa yanayohusiana na lugha hiyo, kwa mfano, viambishi-ngeli katika nomino za pekee: Mifano kutoka katika majina ya mahali katika Kihaya, Michakato ya utohozi wa nomino za Kiswahili katika Kihaya,

Dhima za uradidi katika mawasiliano ya Kihaya, ulinganishi wa michakato ya kifonolojia katika Kinyambo[1] (lahaja ya Kihaya) na Kiswahili na kadhalika.

Makala hii imegawanyika katika sehemu tano: Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambapo mtafiti anaeleza madhumuni ya makala hii, anatoa fasili za dhana zilizojadiliwa katika makala hii. Sehemu ya pili inafafanua nadharia iliyoongoza uchambuzi wa data ya makala hii. Sehemu ya tatu inaeleza mbinu za utafiti. Sehemu ya nne ni uchambuzi wa data kuhusu kufanana na kutofautiana kwa msamiati katika lahaja za Kihamba na Kiziba ambazo ni lahaja za lugha ya Kihaya. Sehemu ya tano ni hitimisho la makala.

**Nadharia ya Utafiti**

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure (1900). Vipengele vinavyorejelewa katika nadharia hii ni *parole* na *langue*. De Saussure anaona kuwa *parole* yaani utendaji ni lugha katika matumizi. *Parole* inahusiana na umilisi wa lugha wa mtu binafsi kwa kila mzungumzaji wa lugha husika. Kila mwanajamii ana ujuzi wa sarufi ya lugha hiyo. Kipengele cha *langue* yaani mfumo-lugha ni kaida zinazoiwezesha lugha kuwepo na kuziwezesha lugha hizo kufanya kazi. *Langue* inarejelea mfumo-lugha mahsusi duniani mathalani Kiingereza na Kiswahili pamoja na maumbo mbalimbali ya lugha hizo. Kwa mujibu wa De Saussure *langue* ni jumla ya msamiati, sarufi, sheria za uundaji wa maneno na sheria za utamkaji. Hivi ni viwango vya lugha vinavyojitokeza katika lugha zote duniani. Kwa mujibu wa nadharia hii utafiti wa lugha lazima uzingatie mfumo wa lugha husika. Kwa vile lugha ni amali ya jamii, basi inahusu makubaliano ya namna lugha hiyo itakavyotumika katika jamii. Watumiaji wa lugha katika jamii huwa na elimu inayowaongoza katika kujua vipengele vya sarufi, msamiati, sintaksia na semantiki pamoja na ufasaha wa lugha husika. Nadharia hii imemsaidia mtafiti kubaini kuwa kwa vile watafitiwa ni wamilisi juu ya sarufi ya lugha ya Kihaya hususan katika lahaja ya Kihamba na Kiziba, basi hata wakisigana katika msamiati wanaendelea kulinda sarufi ya lugha yao. Pia wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba na Kiziba wanao uwezo wa kutumia msamiati tofauti wakirejelea dhana ileile bila kuathiri maana iliyokusudiwa kutokana na uwezo wa kutumia lugha ya mama au ya kwanza.

**Methodolojia**

Mjadala katika makala hii umejiegemeza katika utaamuli na siyo tarakimu kwani umefanywa kwa kuzingatia misingi ya kitaamuli kwa kuwa data iliyotumika imechambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo katika kutimiza malengo husika. Ili kuongeza uthabiti wa data ya utafiti mbinu za kukusanyia data zaidi ya moja zilitumika. Mbinu hizo ni ushuhudiaji, hojaji, usaili na chanzo cha data cha maktabani. Kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti aliweza kushuhudia namna ambavyo wazungumzaji wa Kihamba na Kiziba wanavyoweza kutamka kwa namna tofauti msamiati wenye maana sawa na unaorejelea dhana ileile. Vilevile mtafiti alishuhudia namna ambavyo watafitiwa hao huweza kutamka kwa namna sawa msamiati huohuo na kurejelea dhana ileile. Kupitia mbinu ya hojaji mtafiti aliandaa dodoso kwa kuorodhesha jumla ya msamiati 161 kwa lugha ya Kiswahili na kuwataka watafitiwa kujaza dodoso hilo kwa kutumia lahaja zao. Dodoso hilo liligawiwa kwa atafitiwa 80 na lilijazwa kikamilifu. Kupitia dodoso hili mtafiti alibaini msamiati wenye kufanana na wenye kutofautiana miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba na Kiziba. Mbinu ya usaili ilitumika katika kuwahoji watafitiwa ana kwa ana ambapo watafitiwa walitakiwa waeleze msamiati

[1] Mojawapo ya lahaja za Kihaya inayozungumzwa wilayani Karagwe ambayo ni miongoni mwa wilaya za mkoa wa Kagera.

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.231


wanaoona unarandana na kutofautiana kitahajia/hijai pia hujulikana kama othografia[2] na kimatamshi miongoni mwao. Hii ilimsaidia mtafiti kubaini msamiati mwingi zaidi tofauti na ule ulioorodheshwa kwenye dodoso. Sambamba na mbinu hizi, makala hii pia ni zao la uchunguzi wa kifafanuzi uliofanywa maktabani. Mapitio ya machapisho mbalimbali mathalani, tasnifu, vitabu, tovuti na majarida mbalimbali, yalisomwa na mtafiti ili kupata data inayohusiana na mada inayoshughulikiwa katika makala hii.

**Uchambuzi wa Data**

Katika utafiti huu jumla ya msamiati mia moja sitini na sita (161) wa lugha ya Kihaya ulikusanywa kutoka uwandani. Msamiati huu unatumika katika lahaja zote mbili yaani lahaja ya Kihamba na Kiziba. Kati ya msamiati huu upo unaorandana na upo unaotofautiana kitahajia na kimatamshi. Mtafiti anathibitisha hili kwa uchanganuzi unaooneshwa katika 4.1 na 4.2:

**Msamiati wa Kihaya Unaorandana katika Lahaja ya Kihamba na Kiziba**

Kupitia mbinu ya hojaji, usaili na ushuhudiaji imebainika kuwa pamoja na kwamba baadhi ya msamiati wa lahaja ya Kihamba na Kiziba hutofautiana kitahajia na kimatamshi, pia upo unaorandana kitahajia na kimatamshi. Data yetu inaonesha kuwa msamiati ufuatao unarandana kitahajia na kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja za Kihaya; Kihamba na Kiziba:

**Jedwali Na. 1: Msamiati wa Kihamba na Kiziba Unaorandana**

| **Kihamba** | **Kiziba** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| Abatwazi/abakama | Abatwazi/abakama | Viongozi. |
| Amagufa | Amagufa | Mifupa. |
| Amarwa | Amarwa | Pombe. |
| Ebiinzi | Ebiinzi | Makamasi. |
| Ebireju | Ebireju | Ndevu |
| Ebishabo | Ebishabo | Matope |
| Ebishomo | Ebishomo | kovu analokuwa nalo mtu mwilini mwake baada ya kumtolea mdudu aitwaye funza. |
| Ebisige | Ebisige | Nyusi za jicho |
| Ebyala nshonga | Ebyala nshonga | Sehemu ya juu ya vidole au mwisho wa vidole (eneo zilipo kucha). |
| Eichenza | Eichenza | Chenza |
| Eichunkwa | Eichunkwa | Chungwa |
| Eitaka lyeibumba | Eitaka lyeibumba | Udongo wa mfinyanzi |
| Ekiguyo | Ekiguyo | Kigae. |
| Ekihiso | Ekihiso | Maharage mabichi mathalani, yaliyovunwa hivi karibuni. |

[2] Watafitiwa walifasiliwa maana ya tahajia na othografia kuwa ni utaratibu wa kuandika maneno kwa namna inayokubalika kulingana na mfumo wa lugha husika.

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.231


| | | |
|---|---|---|
| Ekihosho | Ekihosho | Zana ya kuchimbia mazao yaotayo ardhini mfano, viazi vikuu. Pia ni zana ya kuchimbia migomba. |
| Ekileju | Ekileju | Kidevu. |
| Ekilele | Ekilele | Kifaa wakitumiacho wanaume kuwekea pombe. Ni kirefu ikilinganishwa na 'orushubu' na kina shingo ndefu na kitako kipana. |
| Ekilenge | Ekilenge | Unyayo |
| Ekishenge | Ekifuba | Kifua. |
| Ekishenshe | Ekishenshe | Kifaa wanachojifunga kiunoni wacheza ngoma ili kunogesha uchezaji. |
| Ekishushane | Ekishushane | Picha. |
| Ekishwa | Ekishwa | Kichuguu. |
| Ekitetei | Ekitetei | Nyumba za utamaduni wa Kihaya zinazokandikwa udongo pembeni na kuezekwa kwa nyasi. Mara nyingi huwa za mviringo. |
| Ekyai | Ekyai | Kamba ya mgomba. |
| Ekyalo | Ekyalo | Kijiji. |
| Ekyasha | Ekyasha | Pengo. |
| Ekihoroni/eky'oroni | Ekihoroni/eky'oroni | Choo. |
| Elongolo | Elongolo | Zawadi. |
| Embile/enkundi | Embile | Aina zote za ndizi zinazotumika kutengenezea pombe. |
| Emihanda etana | Emihanda etana | Njia panda. |
| Emigani | Emigani | Hadithi. |
| Emirundi/amagulu | Emirundi/Amagulu | Miguu |
| Empaka | Empaka | Ubishi |
| Empapulo | Empapulo | Kurasa, kwa mfano, kurasa za kitabu. |
| Empashana | Empashana | Makutano ya matawi mawili au zaidi, pia makutano ya vidole. |
| Empaya | Empaya | Beberu/mbuzi dume |
| Empiita | Empiita | Jasho. |
| Empunu | Empunu | Nguruwe |
| Empurutulilo | Empurutulilo | Fundo lililofungwa. |
| Enaku | Enaku | Umaskini wa kipato/ufukara |

| | | |
|---|---|---|
| Enda | Enda | Mimba |
| Endimu | Endimu[3] | Limau |
| Endulu | Endulu | Yowe/ukunga |
| Enfuka | Enfuka | Jembe. |
| Engai | Engai | Kasia. |
| Engemu | Engemu | Mgomba/migomba |
| Engozi | Engozi | Mbeleko |
| Enjangwa | Enjangwa | Paka. |
| Enjoge | Enjoge | Aina ya ndizi ndefu kwa umbo zinazoliwa zikiwa mbivu. |
| Enjwajwa | Enjwajwa | Udenda. |
| Enkaito | Enkaito | Kandambili zilizotengenezwa kwa taili la gari. |
| Enkokola | Enkokola | Kumbo/ungio lililo katikati ya mkono. |
| Enkokolomi | Enkokolomi | Jogoo. |
| Enkuba | Enkuba | Radi. |
| Enkurungo | Enkurungo | Jiwe la kusagia nafaka, mathalani, uwele, mtama nakadhalika. |
| Enkwi | Enkwi | Kuni. |
| Enkyakya | Enkyakya | Machacha. |
| Enshalazi | Enshalazi | Aina ya matunda madogomadogo yanayopatikana kwenye matawi ya mti mkubwa. |
| Enshanani | Enshanani | Mwanya. |
| Enshenya | Enshenya | Kuku jike/tembe/tetea. |
| Enshundo | Enshundo | Ugonjwa wa ngozi ambapo vidude vigumu na vidogovidogo mithili ya upele hujitokeza juu ya ngozi. |
| Ensindizi | Ensindizi | Bundi. |
| Entubu | Entubu | Jina litamkwalo badala ya kutaja sehemu za siri moja kwa moja. |
| Enumi | Enumi | Fahali/ng'ombe dume. |

[3] Wazungumzaji wa Kihaya wakisema ndimu humaanisha kile kiitwacho limau katika Kiswahili. Aidha, katika lugha hii ya Kihaya, hakuna msamiati wa limau kwani nomino zote hizi mbili (limau na ndimu) hurejelewa na nomino moja ya ndimu katika lugha hiyo.

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.231


| | | |
|---|---|---|
| Enyawawa | Enyawawa | Aina ya ndege mkubwa mithili ya bata isipokuwa yeye huruka angani na hukaa juu ya miti. Kwa imani za Wahaya, ndege huyo akilia mara kwa mara karibu na familia fulani, huashiria kifo cha mtu katika familia. |
| Enyindo | Enyindo | Pua. |
| Ensimbu | Ensimbu | Kifafa. |
| Hangara | Hangara | Neno aambiwalo kiongozi kama kumwambia ajisikie nyumbani. |
| Kuringa ensenene | Kuringa ensenene | Tendo la kwenda mbugani kuangalia kama kuna senene. |
| Mushonge | Mushonge | Nyumba iliyotengenezwa kwa nyasi kuanzia chini hadi juu bila kukandikwa udongo. |
| Obugwa izoba | Obugwa izoba | Kuchwa kwa jua. |
| Obukuutu | Obukuutu | Utukutu. |
| Obumaza | Obumaza | Uthubutu. |
| Obunana | Obunana | Ndizi mbivu fupi kwa umbo na huliwa zikiwa mbivu. |
| Oburo | Oburo | Uwele. |
| Obuunge | Obuunge | Aina ya kamba itumikayo kuunganishia ukili ili kupata mkeka. Huwekwa kwenye sindano na kuushona ukili kwa kuunganisha mithili ya kushona nguo. |
| Obwamba | Obwamba | Damu. |
| Obwato | Obwato | Mtumbwi. |
| Okubaija | Okubaija | Tendo la kutoa magome ya mti kwenye mti. |
| Okugooka | Okugooka | Kuaibika. |
| Okuharuka | Okuharuka | Kuharisha. |
| Okuharula | Okuharula | Kuparua. |
| Okuhura | Okuhura | Mama mwenye mimba kuchukia baadhi ya vyakula, watu, vitu, nakadhalika. |
| Okujunga | Okujunga | Tendo la kutengeneza pombe. |
| Okukabaituka | Okukabaituka | Kugalagala |

| | | |
|---|---|---|
| Okukyala | Okukyala | Kutembelea sehemu/eneo fulani au kumtembelea mtu, uzuru. |
| Okunuga | Okunuga | Kunyali. |
| Okupokya | Okupokya | Kufumba na kufumbua macho. |
| Okusa | Okusa | Kusaga. |
| Okushaala | Okushaala | Hali ya kitu kinachopikwa kupata joto na kukaribia kuchemka. |
| Okushala emambya | Okushala emambya | Mawiyo au Kupambazuka. |
| Okushalala | Okushalala | Kufa ganzi. |
| Okusheshemukwa | Okusheshemukwa | Hali ya kuwa na kichefuchefu. |
| Okubaazira | Okubaziira | Kushona. |
| Okushungamiliza | Okushungamiliza | Kuchuchumaa. |
| Okutanaka | Okutanaka | Kutapika. |
| Okutogosa | Okutogosa | Kuchemsha kitu au chakula motoni. |
| Okutongya | Okutongya | Kuomboleza. |
| Okwebuga | Okwebuga | Kutongoa. |
| Okwegajaibura | Okwegajaibura | Kukaa ovyo ovyo bila nidhamu. |
| Okwegashaniza | Okwegashaniza | Kusali. |
| Okwiyukya | Okwiyukya | Kupongeza. |
| Oluhi | Oluhi | Kofi. |
| Olwazi | Olwazi | Mawe yaliyojitandaza kama mkeka. Wahaya hutumia maeneo haya kwa ajili ya kuanika nguo, kusagia nafaka, na kadhalika. |
| Omuangazima | Omuangazima | Upinde. |
| Omugurusi | Omugurusi | Mwanaume mzee au mzee wa kiume. Pia ni jina analopewa baba na wakwe zake. Haijalishi ni mzee au kijana ilimradi ni baba mkwe. (kwa pande zote mbili, kwa mwanamke na kwa mwanaume) |
| Omugusha | Omugusha | Mtama. |
| Omukaikuru | Omukaikuru | Ajuza |

| | | |
|---|---|---|
| Omulili | Omulili | Mchicha. |
| Omunyakwawa | Omunyakwawa | Kwapani. |
| Omushokoro | Omushokoro | Mboga za majani zitokanazo na majani ya mmea wa maharage. |
| Omusomoro | Omusomoro | Majani yatumikayo kusugulia vyombo badala ya 'steel wire'. Yana makali kama 'steel wire'. |
| Omutoro | Omutoro | Mchezo wa nyimbo na majigambo ambapo wachezaji hushika fimbo na kuvaa nguo maalumu na hujigamba huku wakicheza. |
| Omuyo | Omuyo | Kisu. |
| Oruganda – | Oruganda | Ukoo. |
| Oruhara | Oruhara | Kipara |
| Oruhaso | Oruhaso | Kifaa mithili ya kisu kinachochongwa kwa kutumia kipande cha mti ambapo hutumika kumenyea ndizi. |
| Oruhiila | Oruhiila | Majivu ya nyasi zilizounguzwa kwa moto. |
| Orushubu | Orushubu | Kifaa wakitumiacho wanawake kuwekea pombe. Ni kifupi ikilinganishwa na 'ekilele' na kina shingo fupi na kitako kipana. |
| Orutigongo | Orutigongo | Uti wa mgongo. |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, (2023)

Kama data yetu inavyoonesha katika Jedwali Na. 1 hapo juu, kupitia mbinu ya ushuhudiaji, hojaji na usaili imebainika kuwa lahaja za Kihaya; Kihamba na Kiziba, zimesheheni msamiati unaorandana. Matokeo yanaonesha pia kuwa 75% ya msamiati wa Kihamba na Kiziba hurandana. Aidha, imebainika kuwa lahaja zote mbili huweza kutumia misamiati miwili inayorejelea dhana ileile na inayorandana kiothografia/hijai na kimatamshi. Kwa mfano, *abatwazi* na *abakama* hurejelea viongozi katika lahaja zote mbili. Halikadhalika maneno *emirundi* na *amagulu* (miguu) hutumika katika lahaja za Kihamba na Kiziba.

**Msigano wa Msamiati wa Kihaya katika Lahaja ya Kihamba na Kiziba**

Matokeo ya Makala hii yanabainisha msigano katika lahaja hizi. Isipokuwa msigano huu mdogo hauwafanyi wazungumzaji hawa kutokuelewana kwani pamoja na kutofautiana kiothografia/kihijia katika baadhi ya msamiati huo, bado huelewana na kutambua dhana inayorejelewa kama inavyojitokeza katika mifano:

**Jedwali Na. 2: Msigano wa Msamiati wa Kihamba na Kiziba**

| **Kihamba** | **Kiziba** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| Amasi**ma** | Ama**tu**si | Matuta. |
| Buto**no**/ enkeremeke | Buto**go**/enkeremeke | Mtoto mchanga. |
| Ebigando | Ebilibwa | Mihogo. |
| Ebigi**no** | Ebigi**gy**o | Magego (meno makubwa ya nyuma kuelekea kooni). |
| E**bi**goye | Ebigoye/**en**goye | Marando. |
| Ebiise | Ebyenju/ebiise | Ndizi mbivu. |
| Ebikondo | Ebiko**ro**nd**o**lo | Makohozi. |
| Ebikoronto | Enkaraito | Aina ya matunda meusi, madogo huota mbugani. |
| Ebineno | Ebihendwa | Maharage machanga ambayo hayajakomaa. |
| Ebishuni | Ebi**nyamu**shuni | Aina ya upele, ila huu ni mkubwa. |
| Ebisika | Enkyakya | Tendo la miguu kupasuka sehemu za unyayo au machacha makubwa ya unyayoni na kwenye kisigino |
| Ebyele | Ebihere/ebizimba | Vidonda |
| E**i**bombo | Ebombo | Kaptula |
| Ekigusha | Ekitenge | Muwa |
| **E**kilamura | Ekilamura/**omu**lamura | Aina ya mmea utumiwao kutenganisha eneo la mtu na mtu au maeneo ya watu mbalimbali. |
| Ekishato | Ekishenshe | Nguo iliyochanika. |
| **Ekishenge**/ekifuba | Ekifuba | Kifua. |
| **Akakongoij**orya | **Ekisinjog**orya | Kisigino. |
| Ekiteega | Okujwi | Ungio la paja na sehemu ya chini ya mguu, nyuma ya goti. |
| Ekoko | Enkanja | Mataputapu ya pombe. |
| Embile/embire/**enkundi** | Embile/embire | Aina zote za ndizi zinazotumika kutengenezea pombe. |
| Emila | Embunza | Funza. |
| Empambo | Enono | Kucha. |
| Emparuk**i**/**emparata** | Emparuk**e** | Uharo. |
| Empelege | ebihimba | Maharage |
| Endyamiti | Embaizi | Shoka. |
| Enfuma | Ebitakuli | Viazi. |
| Engal**a**nyuma | Engal**o**nyuma | Tendo la kupiga kofi kwa kutumia sehemu ya nyuma ya kiganja. |

| | | |
|---|---|---|
| Enkoj**o** | Enkoj**u** | Kovu. |
| Enko**kobya** | Enko**ndo** | Sehemu ya kijiti iliyojikunja kama sehemu ya juu ya mkwaju. Mara nyingi hutumika kusogeza tawi la mbuni ili kumrahisishia mvuna kahawa katika harakati za kuvuna kahawa. |
| E**n**s**e**isa | Es**h**is**h**a | Aina ya kamba zinazotumika kutengeneza 'ekishenshe' wanachojifunga kiunoni wacheza ngoma ili kunogesha uchezaji. |
| Entuntun**wa** | Entuntun**u** | Aina ya matunda ya njano yakiwa yameiva na kijani yakiwa mabichi. |
| Enyatwa | Enya**n**twa | Chuchu. |
| Enzir**a**nyungu | Enzir**o**nyungu | Masizi. |
| Kwita/**kwonja** ebituzi | Kwita ebituzi | Utafutaji wa uyoga mbugani. |
| Okutanaka/**okutabika** | Okutanaka | Kutapika. |
| Olupanka | Ekiso | Panga. |
| Omujuzi | Eshweta | Sweta. |
| Omwend**o** | Omwend**a** | Nguo. |
| Oru**bugu** | Oru**wi** | Ngozi ya mnyama iliyochunwa. |
| Oru**h**oile | Oru**w**oile | Mimba iliyobebwe kabla ya mbebaji kuingia katika ndoa. Maana yake mbebaji (msichana) huyo hubeba mimba ilhali akiwa bado anaishi kwao au kwake pasipo kuolewa. |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, (2023)

Data ya makala hii inabainisha kuwa pamoja na kwamba lahaja ya Kihamba na Kiziba zina msamiati unaorandana, pia lahaja hizi zina msamiati unaosigana kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 2 hapo juu. Aidha, inaonesha kuwa 25% ya msamiati wa lahaja hizo husigana ilhali 75% ni kwa msamiati unaorandana kama ilivyo katika Jedwali Na. 1. Pia matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa lahaja zote mbili huweza kutumia misamiati miwili inayorandana kiothografia/hijai na kimatamshi ikirejelea dhana moja. Kwa mfano, msamiati *abatwazi* na *abakama* ambayo inarejelea viongozi, hutumika katika lahaja za Kihamba na Kiziba. Maneno *emirundi* na *amagulu* (miguu) pia yanatumika katika lahaja hizi mbili.

Aidha, matokeo ya uchanganuzi wa data yanabainisha kuwa wakati mwingine mojawapo ya lahaja huwa na msamiati zaidi ya mmoja ilhali lahaja nyingine ina msamiati mmoja na misamiati yote hurejelea dhana moja. Mathalani, katika lahaja ya Kihamba msamiati *okutanaka* na *okutabika* hurejelea tendo la kutapika ilhali katika lahaja ya Kiziba unatumika msamiati *okutanaka* pekee. Vilevile

msamiati *kwita* na *kwonja* ebituzi unaorejelea tendo la kutafuta uyoga mbugani unatumika katika lahaja ya Kihamba ilhali katika lahaja ya Kiziba unatumika msamiati *kwita* ebituzi pekee.

**Sababu za Kufanana na Kutofautiana kwa Baadhi ya Msamiati wa Kihamba na Kiziba**
Uchanganuzi wa data ya makala hii unaonesha kwamba baadhi ya msamiati wa Kihamba na Kiziba hurandana na baadhi husigana. Sababu[4] za kufanana kwa baadhi ya msamiati wa lahaja hizi ni kutokana na sababu kuwa lahaja hizi zina msingi mmoja wa lugha mama ambayo ni Kihaya. Halikadhalika, wazungumzaji wa lahaja hizi wanaishi katika mwambao wa ziwa Viktoria. Hivyo, lahaja hizi zina mwingiliano mkubwa kutokana na ukaribu uliopo baina ya wazungumzaji wake. Ukaribu huu husababisha wahusika kuwa na msamiati mwingi unaorandana, utamaduni, mila, desturi na itikadi zinazoendana. Halikadhalika, baadhi ya msamiati wa lahaja hizi husigana kutokana na umbali wa kijiografia kati ya Wahamba waishio maeneo ya Kyamutwala na Waziba waishio maeneo ya Kiziba. Japokuwa wote wanapatikana katika mwambao wa Ziwa Viktoria, lakini wako maeneo tofauti. Mathalani, Wahamba wanapatikana Kusini mwa mkoa wa Kagera na Waziba wako Kaskazini mwa mkoa huu. Kama ilivyoelezewa katika 1.2 kuwa mkoa wa Kagera kwa upande wa Kaskazini unapakana na Uganda, basi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kihaya wanaoishi Kaskazini mwa mkoa wa Kagera ni Waziba ambao lahaja yao ni Kiziba. Hivyo, data ya makala hii inadhihirisha wazi kuwa wenyeji wa Uganda wanaozungumza lugha ya Kiganda (Luganda) ndiyo wenye mtagusano mkubwa na Waziba. Aidha, mtafiti alishuhudia wakazi wa Kiziba wakivuka kwa mitumbwi kuelekea Uganda kupitia Minziro (japokuwa alielezwa kuwa njia hii si rasmi). Hii inadhihirisha wazi kuwa kuna mtagusano mkubwa miongoni mwao hali inayosababisha kuathiriana kwa Kiziba na Kiganda. Kwa upande mwingine, msamiati wa lahaja hizi husigana kutokana na mwingiliano kati ya Waziba na Waganda waishio Uganda.

**Hitimisho**
Makala hii inadhihirisha kuwa kuna kufanana kitahajia/hijai na kimatamshi kwa baadhi ya msamiati wa lahaja hizi lakini pia zipo tofauti za kitahajia/kiothografia na kimatamshi kwa baadhi ya msamiati miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba na Kiziba. Aiodha, matokeo ya makala hii yanadhihirisha wazi pia kuwa lahaja zote mbili huweza kutumia misamiati miwili inayorejelea dhana ileile na inayorandana kiothografia/kitahajia na kimatamshi. Kwa mfano, *abatwazi* na *abakama* hurejelea viongozi, pia misamiati *emirundi* na *amagulu* inayorejelea miguu hutumika katika lahaja zote mbili, Kihamba na Kiziba. Halikadhalika, matokeo ya makala hii yanabainisha kuwa wakati mwingine mojawapo ya lahaja huwa na msamiati zaidi ya mmoja ilhali lahaja nyingine ina msamiati mmoja na misamiati yote mitatu hurejelea dhana ileile. Kwa mfano, katika lahaja ya Kihamba msamiati *embile* na *enkundi* hurejelea aina zote za ndizi zinazotumika kutengenezea pombe ilihali katika lahaja ya Kiziba unatumika msamiati *embile* pekee. Vilevile msamiati *Ebigoye* na *engoye* unaorejelea marando, unatumika katika rahaja ya Kiziba ilhali katika lahaja ya Kihamba unatumika msamiati *ebigoye* pekee. Inapendekezwa utafiti wa kina zaidi ufanyike kuhusiana na sababu za kutofautiana na kufanana kwa msamiati wa lahaja hizi. Aidha, makala hii itatoa hamasa kwa watafiti

[4] Kiukweli sababu za kufanana na kutofautiana kwa baadhi ya msamiati wa lahaja ya Kihamba na Kiziba ni suala linalohusisha historia ya wazungumzaji wa lahaja hizi kuhama kutoka eneo moja hadi jingine, mwingiliano wao na wazungumzaji wa lugha nyingine, mipaka ya nchi moja na nyingine mathalani Tanzania, Uganda na Rwanda na Burundi. Hivyo, katika makala hii tumeandika kwa ufupi sana na kutoa mwanya kwa tafiti nyingine kushughulikia suala hili kwa kina.

kufanya tafiti juu ya lahaja za lugha mbalimbali. Vilevile, makala hii inatoa mchango katika kukuza na kuendeleza lugha za Kibantu na taaluma ya isimu kwa ujumla.

## Marejeleo

Abdalla, M. M. (2018). "Udondoshaji katika Lahaja za Pemba". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Adolph, E. (2014). "Utohozi wa Nomino za Kiswahili na Athari yake katika Ngeli za Kihaya". Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Adolph, E. (2022). "Dhima za Uradidi katika Mawasiliano ya Kihaya". Katika Mwanga wa Lugha. *Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Moi*. Juzuu 6 Na. 1. Uk. 159-170.

Akmajian, A., Demers, R. A., Farmer, A. K. & Harnish, R. M. (2001). Linguistics: An Introduction to Language and Communication, Toleo la 5. USA: Massachusetts Institute of Technology.

Buberwa, A. (2011). "Viambishi-Ngeli katika Nomino za Pekee: Mifano kutoka katika Majina ya Mahali katika Kihaya". Katika *Kiswahili*. *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. Juz. 74, uk. 41-48.

Buberwa, A. (2015). Mofolojia ya Majina ya Mahali ya Kiswahili na Kihaya katika Jamii ya Wahaya: Uzingativu wa Masuala ya Kiisimujamii. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Byarushengo, E. (1997). *Haya Grammatical Structure Phonology, Grammar and Discourse*. Published by the Department of Linguistics University of Southern California Los Angeles; California.

Chiraghdin, S. & Mnyampala M. E. (1977). Historia ya Kiswahili, Nairobi: Oxford University Press.

France, B & Kahigi, K. K (2001). Ulinganishi wa Michakato ya Kifonolojia katika Jarida la Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA Journal). Juzuu 3 Na. 3. Uk. 134-155.

Francis, W. N. (1992). "Dialectology", katika W. Bright (Mhariri), International Encyclopedia of Linguistics, 349–355. Oxford: Oxford University Press.

Hamad O. S. (2018). "Ulinganishi wa Njeo na Hali katika Lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Ingrams, W. H. (1924). The Dialects of the Zanzibar Sultanate in Bulletin of the School of Oriental and African Studies, Vol.III, Part III. London. (pp 533- 550).

Kipacha, A. (2003). "Lahaja za Kiswahili". Chuo Kikuu Huria Dar es Salaam. Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004) Kamusi Ya Isimu Na Falsafa ya Lugha. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mgullu, R. S. (1999). Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili Nairobi Kenya, Longhorn Publishers

Muhura, C. (2009). Kiswahili – Lugha na Fasihii kidato cha 3, Dar es Salaam. Kiiya Publishers.

Mutembei, A. K (2001). *Poetry and AIDS in Tanzania: Changing Metaphors and Metonymies in Haya Oral Traditions*. The Netherlands: Leiden University.

Nurse, D. & Spear, T. (1985). *The Swahili. Reconstructing the History and Language of an African Society*, 800-1500. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

O'Grady, W., Drobovosky, M. na Katamba, F. (2001). Contemporary Linguistics (4th ed.). Bedford/St. Martin's Press. Boston.

Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English (2000), Oxford University Pree Nairobi

Stigand, C. H. (1915). *A Grammar of Dialectical Changes in the Kiswahili Language*. Cambridge At the University Press.

Stigand, C. H. (1915). Dialects in Swahili. Cambridge University.

Whiteley, W. (1956) "Ki- mtang‟ata (A Dialect of the Mrima Coast -Tanganyika)". Kampala. East African Swahili Committee.

Wikipedia, (2021). "Lahaja za Kiswahili – Kamusi Elezo Huru". https://sw.m.wikipedia.org. Imesomwa tarehe 24/5/2023.